OVERLAND HIGH SCHOOL
Marumbo - KISARAWE
P.O. Box 28098, Kisarawe or P.O. Box 10901 Dar es Salaam
Tel: 0754 788644 / 0784 788644
E-mail: overlandhighschool@yahoo.com
...quality and affordable education

*Tovuti: www.overlandhighschool.co.tz*

KWA MZAZI/MLEZI WA…………………………………… TAREHE ………………..

# MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA OVERLAND HIGH SCHOOL MWAKA 20… (JOINING INSTRUCTIONS)

Tunayo furaha kukujulisha kwamba kijana wako …………………………………. amechaguliwa kujiunga na kidato cha………….. mwaka wa masomo …………………. katika shule yetu ya Overland High School (OHS). HONGERA!

OHS iko katika Mkoa wa Pwani Wilaya ya Kisarawe na imesajiliwa na Serikali kwa namba S.3856. Pia imeidhinishwa kuwa Kituo cha mitihani ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) kwa namba S.3811 kwa watahiniwa wa shule na kwa namba P.3811 kwa watahiniwa wa kujitegemea. Shule ipo umbali wa kilometa 45 kutoka Kisarawe Mjini.

**Shule ya Sekondari ya Overland ni ya Bweni tu.**

**Shule itafunguliwa rasmi siku ya ………………. tarehe …………………, 20…..**

Kwa wanafunzi wanaojiunga mwanzo wa mwaka wa masomo, usafiri wa jumla utaanzia Gongo la Mboto saa tano asubuhi tayari kwa safari ya kuelekea shuleni. Kila mwanafunzi atapaswa kuja na nauli yake mkononi ya shilingi................kwa sasa.

Atakayechelewa au anayehamia baada ya muhula wa masomo, itampasa kwenda Kigogo Fresh (Chanika), kituo cha mabasi yaendayo **MSANGA,** na akiwa kwenye basi hilo la **Msanga**, itambidi amwelekeze Kondakta amshushe kwenye kituo cha **MFURU**. Hapo kituoni Mfuru atapata usafiri mwingine wa kufika shuleni, Overland High School.

Baada ya kufika shuleni, wanafunzi wote wanapaswa kuripoti katika ofisi ya UTAWALA na UHASIBU wakiwa na mizigo yao yote zikiwemo Hati ya Malipo ya Benki *(Bank pay in slips)* za malipo kamili ya ada ya muhula husika kwa ukaguzi na hatimaye kupokelewa mabwenini.

**Maelekezo kwa wanafunzi wanaohamia OHS**

Mwanafunzi anayehamia OHS atapokelewa shuleni kwetu wakati wowote. Hata hivyo atapaswa hatimaye kuleta Hati za Utambulisho kutoka shule aliyohama ili kukamilisha usajili.

**Malipo ya Ada, Sare na Gharama nyingine:-**

Hakikisha malipo ya muhula wa kwanza yalioonyeshwa hapa chini yanalipwa kabla ya kuripoti shuleni kuepukana na hatari ya mtoto wako kupoteza nafasi ya masomo aliyopewa katika shule yetu ya Overland High School. **MALIPO YOTE YAFANYIKE KUPITIA BENKI.** Hati ya malipo (Bank pay in slip) yenye **jina la mwanafunzi** na kidato anachosoma iletwe shuleni siku ya

kuripoti, kwenye ofisi ya Uhasibu. Hakikisha unapata hati ya malipo (risiti) ya shule. Malipo kwa kutumia hundi (cheque) binafsi hayapokelewi.

Kwa mwanafunzi anayehamia malipo ya ada yataanzia tarehe anayoripoti shuleni na kuendelea kulipa kwa mchanganuo uliopo hapo chini.

**MCHANGANUO WA MALIPO KWA KIDATO CHA KWANZA MPAKA CHA SITA.**

| S/N | | JUMLA | AWAMU YA 1 JAN - MAR | AWAMU YA 2 APR - JUN | AWAMU YA 3 JUL - SEPT | AWAMU YA 4 OCT - DES |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada | 2,150,000 | 550,000 | 550,000 | 550,000 | 500,000 |

**MAHITAJI YA LAZIMA KWA MWAKA WA KWANZA WA MASOMO.(Mwanafunzi Mpya)**

| S/N | | JUMLA | AWAMU YA 1 JAN - MAR | AWAMU YA 2 APR - JUN | AWAMU YA 3 JUL - SEPT | AWAMU YA 4 OCT - DES |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Sare | 100,000 | 100,000 | - | - | - |
| 2 | Kitambulisho | 15,000 | 15,000 | - | - | - |
| 3 | Tshirts | 25,000 | 25,000 | - | - | - |
| 4 | Nembo | 20,000 | 20,000 | - | - | - |
| 5 | Uniform za Michezo | 25,000 | 25,000 | - | - | - |
| 6 | Umiseta | 5,000 | - | 5,000 | - | - |
| 7 | Matibabu | 60,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| 8 | Stationary | 30,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | - |
| 9 | Vifaa vya Usafi | 10,000 | 5,000 | - | 5,000 | - |
| 10 | Maabara | 40,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 11 | Godoro | 40,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 12 | Tahadhari/Uchakavu | 40,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 13 | Shamba Dress | 60,000 | 60,000 | - | - | - |
| | **JUMLA** | **470,000** | **305,000** | **60,000** | **60,000** | **45,000** |

**TAARIFA ZA AKAUNTI YA SHULE YA KUFANYIA MALIPO.**

| Akaunti ya Benki | Jina la Benki | Jina la Akaunti |
|---|---|---|
| **21406600007** | **NATIONAL MICROFINANCE BANK (NMB)** | **OVERLAND HIGH SCHOOL** |

**TANBIHI:**

1. Malipo ya mitihani ya taifa (NECTA, MOCK, n.k) yatalipwa na mwanafunzi kulingana na kiwango cha wakati huo kitachowekwa na mamlaka husika.

2. Fomu ya maombi ya kujiunga na shule inauzwa shilingi 15,000/= tu (usaili).

3. Kidato cha kwanza mpaka cha nne (O-level):Mwanafunzi aje na Sweta ya rangi ya MARUNI(damu ya mzee)

4. Kidato cha tano mpaka cha sita (A-level):Mwanafunzi aje na Sweta ya rangi ya KIJIVU.

5. Tafadhali zingatia endapo sare ya mwanafunzi itachakaa ama kutomtosha hapo baadaye, itakuwa ni wajibu wa Mzazi/Mlezi kumshonea mtoto sare mpya.

6. Wakati wa michezo ni lazima mwanafunzi avae nguo za michezo na viatu ambavyo inabidi umnunulie. (Viatu vya michezo ni rangi nyeupe mchanganyiko na blue)
7. UMISETA inachangiwa Sh.5,000 kwa mwaka.

8. Nguo za nyumbani hazitoruhusiwa kabisa kuonekana katika mazingira ya shule au bwenini.

9. Suruali za kubana (Model) hazitaruhusiwa. Endapo utashona suruali ya kubana itahesabika kuwa ni nguo ya nyumbani vile vile na itachomwa moto

10. Shule inatoa matibabu ya awali. Kwa matibabu zaidi nje ya shule, mzazi itampasa kugharamia. Mchango wa matibabu ya awali ni Sh.60,000 kwa mwaka.

11. Mwanafunzi wa mchepuo wa Sanaa kwa ngazi ya ‘A’ (level) hatochangia huduma ya Maabara.

12. Ada ya shule na malipo mengine **LAZIMA** yalipwe kupitia kwenye akaunti ya Benki iliyotajwa hapo juu, na hati ya malipo hayo iletwe shuleni kwa ajili ya kupatiwa risiti.

13. Jaza kikamilifu fomu zilizoambatanishwa na barua hii na uje nazo shuleni siku ya kuripoti. Hutasajiliwa kama utakuja na fomu ambayo haijakamilika.

14. Anatakiwa awe na nakala ya cheti cha kuzaliwa pamoja na picha ndogo **(passport size) nne (4),** moja ibandikwe kwenye fomu Ukurasa wa **8 (TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI)**, na tatu (3) ni kwa matumizi ya ofisi.

15. Anatakiwa kuwa na vitu binafsi vyote kama vilivyodhoreshwa hapa:
    - Biblia Tatakatifu (kwa wakristu)
    - Quaran Tukufu (kwa waislamu)
    - Dictionary – Oxford Advanced Learners (kwa wote)
    - Mathematical Set (Oxford) kwa wote.

16. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa malipo yote yamefanyika kikamilifu, yaani kwa wakati unaotakiwa na kiasi kinachotakiwa.

17. Masuala ya usajili na taarifa za malipo, yapo moja kwa moja chini ya Mkuu wa Shule.

**VITU BINAFSI AMBAVYO MWANAFUNZI ATATAKIWA KUJA NAVYO SHULENI NI:-**

1. Jozi mbili za shuka (Pinki kwa Wasichana na Blue kwa Wavulana).
2. Taulo moja.
3. Nguo za kulalia.
4. Truck suit (1 pair) rangi ya kijivu.
5. Jozi tatu za soksi nyeupe.
6. Jozi moja ya malapa.
7. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi.
8. Jozi moja ya viatu vya michezo.
9. Vibanio vya kuanikia nguo.
10. Brashi na Rangi ya viatu nyeusi **-** *(inapatikana kwenye duka la shule).*
11. Sabuni za kuogea na kufulia - *(inapatikana kwenye duka la shule).*
12. Mafuta ya kujipaka (Vaselline) -- *(inapatikana kwenye duka la shule).*
13. Dawa na Brashi ya meno - *(vinapatikana kwenye duka la shule).*
14. Tochi.
15. Exercise Books (Counter books 4Q) - *(zinapatikana kwenye duka la shule).*
16. Kamusi (Kiswahili au/na Kiingereza).

17. Mathematical tables (Booklet).
18. Mto wa kulalia.
19. Sanduku la nguo la chuma *(Truncker with pad lock).*
20. Kolabo moja na kijiko kwa ajili ya chakula na Mug moja kwa ajili ya chai.
21. Awe na vitabu vyake binafsi. Vitabu hivyo ni kama atakavyoelekeza Mwalimu wa somo husika.

**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi kutumia aina ye yote ya dawa za nywele au kemikali yoyote.

## SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KWA WANAFUNZI

### KUWAHI SHULENI

1. Kila mwanafunzi ni lazima awe tayari kwa masomo saa 1.30 asubuhi
2. Mwanafunzi ni lazima awe ameingia na kukaa katika kiti chake kabla ya mwalimu wa somo kuingia darasani na kuanza kufundisha.
3. Wanafunzi wote ni lazima wawe kimya wakimsikiliza mwalimu wakati akifundisha isipokuwa mwalimu akiuliza swali, akiruhusu mjadala au maigizo darasani.

### USAFI NA KAZI ZA MIKONO

1. Kila mwanafunzi ni lazima avae sare safi za shule na aonekane nadhifu wakati wote
2. Kila mwanafunzi atashiriki katika kusafisha na kutunza mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kufagia/kudeki vyumba vya madarasa, mabweni, vyoo na mazingira ya shule kwa ujumla.
3. Kila mwanafunzi atashiriki katika kazi za mikono (bustani na shamba) na lazima atunze vyombo vya shule vya kufanyia kazi (mfano fyekeo, jembe, reki, n.k) na upotevu wa vyombo hivi utagharamiwa na mwanafunzi ambaye atakuwa amehusika katika upotevu wa chombo/vyombo hivyo.

### NIDHAMU

1. Mwanafunzi anatarajiwa kuwa na heshima kwa wanafunzi wenzake, wafanyakazi wote wa shule na wageni wote anaokutana nao awapo shuleni au sehemu nyingine yoyote ile.
2. Mwanafunzi anatarajiwa kupokea maelekezo, maagizo na amri zinazotolewa na uongozi wa shule na serikali ya wanafunzi bila ubishi.
3. Mwanafunzi hategemewi kutumia lugha ya matusi kwa wanafunzi wenzake au mtu mwingine yeyote yule.
4. Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki na kutumia simu za mikononi, radio za mifukoni, mikufu ya aina yoyote na herein.
5. Ni marufuku kuwa na pesa taslimu, pesa za matumizi zitatunzwa kwenye ofisi ya uhasibu na zitatolewa kwa utaratibu wa shule.
6. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote anapokuwa shuleni (darasani na nje ya darasa).
7. Viatu vya shule lazima viwe vyeusi visivyo na mapambo wala visigino virefu (mabuti hayaruhusiwi).
8. Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na chakula chochote bwenini wala kulia chakula bwenini.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kutumia mishumaa shuleni isipokuwa kwa shughuli za ibada tu kwa wakristu.

### DINI

1. Shule inaruhusu kila mwanafunzi kuabudu kulingana na imani ya dini yake kwa kufuata ratiba na taratibu za shule.
2. Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili dini au dhehebu lake bila ya taarifa rasmi ya maandishi kutoka kwa mzazi/mlezi wake.

## TAALUMA

1. Ni lazima kila mwanafunzi kuwa makini katika masomo yake kwa kutumia vizuri nafasi aliyopata.
2. Mwanafunzi yeyote anayeshindwa kufikia kiwango cha kufaulu cha shule kilichokubaliwa na Bodi ya shule hataruhusiwa kuendelea na kidato kinachofuata. Kiwango hicho kinaweza kubadilika wakati wowote kufuatana na ushauri wa wazazi, walimu na bodi ya shule.
3. Ni lazima mwanafunzi afanye mitihani, majaribio na mazoezi yote anayopewa na walimu wake wa masomo mbalimbali katika muda uliopangwa.
4. Mwanafunzi yoyote ambaye atakosa kuja shule na kuhudhuria darasani kwa muda wa siku kumi na tano (15) baada ya kufungua shule na/au mfululizo kwa siku kumi na tano, atafukuzwa shule.

## WAGENI

1. Wageni hawaruhusiwi kufika shuleni kuonana na mwanafunzi wakati awapo masomoni. Wanafunzi watatembelewa siku maalum iliyopangwa na kwa taratibu za shule. Vyakula vya kupikwa haviruhusiwi shuleni siku ya kutembelea wanafunzi.
2. Taarifa za tatizo lolote lile kutoka nyumbani zitolewe kwa uongozi wa shule na sio mwanafunzi mhusika moja kwa moja. **Namba ya simu ya shuleni ni 0716 82 60 92 au 0759 65 94 55.**

## TABIA NA MWENENDO

1. Ni marufuku kupiga kelele au kuleta usumbufu wa aina yoyote shuleni (darasani, bwenini au nje ya darasa).
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoka nje ya eneo la shule bila ya kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu wa nidhamu, Makamu Mkuu wa shule au Mkuu wa shule.
3. Kila mwanafunzi anawajibika kutunza mali yake binafsi na mali ya shule, na kutoa taarifa kwa utawala wa shule endapo mali hizo zitaharibiwa/kuharibika.
4. Wizi wa aina yoyote hauvumiliki shuleni.
5. Lugha ya mawasiliano wakati wote mwanafunzi awapo shuleni ni Kiingereza, isipokuwa wanapokuwapo tu wageni kutoka nje ya shule.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI MARA MOJA

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Ubakaji pamoja na vitendo vya kujamiiana.
3. Kumiliki na kutumia bangi, sigara, pombe ya aina yoyote pamoja na madawa ya kulevya.
4. Kuiba mitihani, kutazama mitihani kutoka kwa mwanafunzi mwingine au kuingia kwenye chumba cha mtihani na majibu yaliyoandikwa kwenye mwili, karatasi, nguo, rula, n.k. pamoja na kuongea na mwenzake kwenye chumba cha mtihani bila ya ruhusa ya msimamizi wa mtihani.
5. Kupigana na wanafunzi wenzake au na mtu yeyote.
6. Kutumia lugha ya matusi.
7. Kutoka katika eneo la shule bila ruhusa.
8. Kuhujumu au kuharibu kwa makusudi mali za shule au ya mtu yeyote.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata ujauzito au kumpa ujauzito mtu mwingine.
11. Kujaribu kutoa au kutoa ujauzito.
12. Kuonekana na mwanafunzi wa jinsia tofauti wakati wa usiku sehemu za giza.
13. Kuonekana kwenye nyumba au maeneo ya nyumba za waalimu au za wafanyakazi wengine wa shule bila idhini ya Mkuu wa Shule.

***Kumbuka:*** Shule ina haki ya kubadili sheria hizi wakati wowote ili kulinda nidhamu ya shule.

**KIBALI CHA KUTOKA NJE YA SHULE *(GATE PASS)***

Kutokana na sababu maalum, mwanafunzi anaweza akaruhusiwa kwenda nyumbani, kwa idhini ya mzazi au mlezi na baada ya kupata kibali kutoka kwa Mkuu wa Shule. Mwanafunzi akikutwa nje ya mipaka ya shule bila kibali atakuwa amejifukuzisha shule.

**HITIMISHO**

BAADA YA KUSOMA NA KUELEWA MAELEZO HAYO HAPO JUU, SASA JAZA FOMU ZIFUATAZO KIKAMILIFU NA ZIREJESHWE SHULENI SIKU YA USAJILI WA MWANAO.

**MWISHO**

Kauli mbiu yetu inasema “ELIMU NI URITHI BORA ZAIDI” (Education is the Best Inheritance). Kila mdau wa Elimu, hasa mzazi au mlezi wa mwanafunzi wa Overland High School (OHS) anaombwa akumbuke umuhimu wa kauli mbiu hii kila tunapoongelea maendeleo ya elimu hapa shuleni kwetu.

Wako katika Elimu,

....................................

**MKUU WA SHULE**

OVERLAND HIGH SCHOOL
Marumbo - KISARAWE
P.O. Box 28098, Kisarawe or P.O. Box 10901 Dar es Salaam
Tel: 0754 788644 / 0784 788644
E-mail: overlandhighschool@yahoo.com
...quality and affordable education

PICHA YA MWANAFUNZI YA SASA (PASSPORT SIZE)

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

**A: HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. **(i) Majina matatu ya mwanafunzi**

…..............................................................................................................Jina hili ni **lazima** libaki kama lilivyoandikwa kwa kipindi chote utakachokuwa mwanafunzi wa shule hii.

(ii) Tarehe ya kuzaliwa: ………………………………………………………………

(iii) Wilaya: …………………………… Mkoa: ……………………………………

(iv) Dini: …………………………….. Dhehebu …………………………………….

(v) Shule ulizosoma kabla ya kujiunga na shule hii:

| Jina Uliloandikishwa | Shule uliyosoma | Wilayailipo shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

2. **Afya**

Taja matatizo yako ya afya ambayo unayo kwa sasa. Ambatanisha vyeti vya Daktari.

…………………………………………………………………………………………………….

**NB:** Kwa wale wenye matatizo ya afya yanayohitaji chakula maalumu **(special diet)** hawataweza kumudu mazingira ya shule yetu kwani shule haitoi chakula maalum (special diet).

**B: HISTORYA YA FAMILIA**

1. MAJINA YA WAZAZI/WALEZI:

Baba …………………………………………………*Hai /Amefariki Mwaka…........................
Dini……………………………………… Dhehebu ……………………………………………
Kazi ……………………………………………………………………………………...
Anuani: ……………………………………………………………………………………
Namba ya simu…………………………………………………………………………….

Barua pepe ……………………………………………………………………………....
Fax………………………………………………………………………………………...

Mama ............................................................................................ *Hai/Amefariki Mwaka………............................
Dini…………………………………………………… Dhehebu ………………………………
Kazi ……………………………………………………………………………………...
Anuani: ……………………………………………………………………………………..
Namba ya simu…………………………………………………………………………..
Barua pepe …………………………………………………………………………...
Fax…………………………………………………………………………………….

Mlezi………………………………………………… Uhusiano …………………………......
Dini…………………………………………………… Dhehebu ………………………………
Kazi ………………………………………………………………………………………
Anuani: ……………………………………………………………………………………..
Namba ya simu…………………………………………………………………………..
Barua pepe ……………………………………………………………………………
Fax ……………………………………………………………………………………...

**C: MAWASILIANO KATI YA SHULE NA MZAZI/MLEZI**

Wakati wa likizo fupi au ndefu wanafunzi hawaruhusiwi kubaki shuleni. Mwanangu anaweza kwenda kwa:

Jina………………………………………………… ………………………………………....
Uhusiano …………………………………………………………………………….................
Anuani na namba ya simu………………………………………………………….............
……………………………………………………………………….......................................

**D: TAARIFA ZA ATAKAYEGHARAMIA MASOMO NA MAHITAJI YA SHULE**

Jina …………………………………………………………………………………………………
Uhusiano na mwanafunzi ……………………………………………………………………………
Kazi…………………………………………………………………………………………………
Anuani yake ……………………………………………………………………………………......
Namba ya simu:
Nyumbani:……………………. Ofisini:……………......... Mkononi:…………………......

**RIDHIO**

Mzazi/Mlezi anapoamua kumwandikisha mtoto wake katika shule hii ni lazima aridhie kwamba malipo atakayolipa kwa ajili ya mwanae hayatarejeshwa kwake iwapo:-

(a) ataamua kumhamisha mwanafunzi kutoka shule hii kwa sababui yoyote ile,

(b) mwanafunzi atasimamishwa au kufukuzwa shule.

Kwa kuthibitisha hili, kila mzazi/mlezi ni lazima ajaze sehemu iliyo wazi hapa chini:

Mimi ………………………………………………………………………………………

Mzazi/Mlezi wa …………………………………………………………………………

Naahidi kwamba sitadai malipo niliyomlipia mwanafunzi mwenye jina hilo hapo juu mara nitakapoamua kumhamisha kutoka katika shule hii kwa sababu yeyote ile au iwapo mwanafunzi huyo atasimamishwa au kufukuzwa shule.

Sahihi:………………………………………………..

Tarehe………………………………………………

## TAMKO LA KUKUBALI SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

### A: TAMKO LA MWANAFUNZI LA KUKUBALI SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Nakiri kuwa nimezisoma, nimezielewa na kuzikubali sheria zote za shule kama zilivyoelezwa katika hati hii ya maelekezo ya kujiunga na shule (Joining Instructions). Naahidi kwa dhati kuwa nitazitii, nitazifuata na nitazitekeleza sheria na kanuni hizi kwa moyo wangu wote.

Sahihi ya mwanafunzi : …………………………………… …………………………

Tarehe……………………………….

### B: TAMKO LA MZAZI/MLEZI KUKUBALI SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Nakiri kuwa nimesoma. Nimezielewa na kuzikubali sheria zote za shule kama zilivyoelezwa katika hati hii ya maelekezo ya kujiunga na shule (Joining Instructions). Nathibitisha kuwa nimezisoma na kumfafanulia mwanangu kwa makini. Naahidi kuwa nitatoa ushirikiano wa hali ya juu katika kumhimiza na kumkumbusha mwanangu kuzitii, kuzifuata na kuzitekeleza sheria na kanuni hizi.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: …………………………………………………………………………..

Tarehe: ………………………………………

OVERLAND HIGH SCHOOL
Marumbo - KISARAWE
P.O. Box 28098, Kisarawe or P.O. Box 10901 Dar es Salaam
Tel: 0754 788644 / 0784 788644
E-mail: overlandhighschool@yahoo.com
...quality and affordable education

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be filed by an Authorized Government Medical Officer and returned to School by the student)
SURNAME………………………… OTHER NAMES……………………………………….
AGE………SEX…………………… .CITIZENSHIP………………………………………..

## A. PERSONAL HISTORY

Please indicate ***YES*** or ***NO*** if the student is suffering from any of the following diseases:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 15 | Pneumonia | |
| 2 | Pleurisy | | 16 | Asthenias/Asthma | |
| 3 | Rheumatic Fever | | 17 | Allergy disorder | |
| 4 | Heart Disease | | 18 | Gastric or duodenal | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 19 | Jaundice | |
| 6 | Dysentery | | 20 | Varicose Veins | |
| 7 | Kidney or urinary disease | | 21 | Diabetes | |
| 8 | Epilepsy | | 22 | Deformity | |
| 9 | Psychotic | | 23 | Eye disorder | |
| 10 | Ear, Nose or Throat disorder | | 24 | Skin disease | |
| 11 | Anemia | | 25 | Gynecological disorder | |
| 12 | Malaria/other tropical disease | | 26 | Cholera | |
| 13 | Major/minor operations | | 27 | Serious accidents | |
| 14 | Any other serious disorder | | 28 | Measles | |

**NB:** Any problem must be supported by medical documents.

## B. PHYSICAL EXAMINATION

Height ……………………………………………………………………………………….
Skin disease…………………………………………………………………………………
Eye conjunctivae: Pupils: ………………………………………………………………….
Vision Right: ……………………………………………………….
Vision Left: ………………………………………………………...
Please state condition of: Ear (if any discharge)……………………………………………..
Mouth and throat ……………………………………………
Nose ……………………………………………………..
Any abnormality ………………………………………………………………………..
Cardiovascular system: Blood Pressure: Systolic ………………………………….
Diastolic.…………………………………………………………………………
Heart: Any murmur? ………………………………………………………………….
Arteries and Veins ……………………………………………………………………….

Abdomen ……………………………………………………………………………………...
Hernia…………………………………………………………………………………………
Hydrocele……………………………………………………………………………………..
Liver ………………………………………………………………………………………….
Kidneys ………………………………………………………………………………………
Rectal …………………………………………………………………………………………
Any clinical evidence of hyperacidity or gastric duodenal ulcer? .......................................

**D. LABORATORY:**

Urine Albinum…………………………………………………………………………
Sugar ……………………………………………………………………………
Bilharzias ……………………………………………………………………………
** Stool: Special emphasis on Hookworm or Bilharzias………………………
** Blood examination:

- Hb level…………………………………………………………………
- Neuotrophils …………………………………………………………
- Eusinophils …………………………………………………………..
- Biscophils ……………………………………………………………
- Lymphocites …………………………………………………………
- Monooytes …………………………………………………………..
- ESR ………………………………………………………………
- X – Ray examination: Chest ……………………………………………………………
- Serology: Widal test …………………………………………………………………….
- Pregnancy Test ………………………………………………………………………….

**CONCLUSION**: (cancel what is not needed)

I have examined Mr/Ms …………………………………………………………………

Considered that he/she is not physically and mentally fit to be admitted to secondary school

……………………………………….. ……………………………… ………………………
Name Signature Date

……………………………………….. ……………………………………………..
Title Qualification

Address: …………………………………….
…………………………………………….
…………………………………………….
……………………………………………..
…………………………………………….